الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness




# UJUMBE UNAOBAKIA



# Yaliyomo

**UJUMBE UNAOBAKIA**

MIONGONI MWA DALILI ZA UTUME WAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

UTUME WA MWISHO

REHEMA KWA WALIMWENGU

FURAHA YA MWANADAMU KWA KUTUMWA KWAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

NI UPI UJUMBE ULIOBAKIA?

UJUMBE ULIOBAKIA NDILO UMBILE LA ULIMWENGU

UJUMBE ULIOBAKIA NI DINI YA MANABII NA MITUME WOTE:

UKAMILIFU WA UJUMBE ULIOBAKIA:

MISINGI YA UWEKAJI SHERIA

SIFA ZA UWEKAJI SHARIA WA KIISLAMU:

SHERIA YA KIISLAMU NA KANUNI ZA WANADAMU…TOFAUTI ZILIZOPO:

VYANZO VYA UISLAMU.




# UJUMBE UNAOBAKIA

Kila mwanadamu anapokuwa mbali na uongofu wa mbinguni na ujumbe wa Mitume basi watu hao watagubikwa na kiza, ndio maana akawa anatuma Mtume baada ya Mtume: {Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [4:165];

Hivyo basi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) hamuadhibu yoyote ambaye hajamtumia Mtume: {…Wala Sisi hatuadhibu mpaka tumpeleke Mtume.} [17:15],

Na baada ya kutumwa kwa Issa ('Alayhi salaam), kisha Allah akamnyanyua jamii mbali mbali ya wanadamu zilisumbuka kwa Ujahilia na upotevu, dhuluma na kiza; hivyo dini za Allah zilikumbwa na mabadiliko ya kuchafuliwa mafundisho yake na baadhi ya waovu wakabadilisha akida yake safi ya tawhidi kwa upagani na ushirikina, na kumfanyia Allah jeuri na kusema juu yake bila ya haki, na kwenda kinyume, na dhati yake, wakati huo hakukuwepo na tofauti yeyote baina ya wapagani na Ahlul Kitabu pamoja na waabudu masanamu katika ibada zao na maisha yao.

Nuru ya tawhidi ikawa imepotea katikati ya msongamano huu mkubwa wa ushirikina na upingaji na kubadilisha na kugeuza maneno ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala), wale waliopewa kitabu wakatupa ahadi na



makubaliano (agano), mikataba na maneno ya Allah nyuma ya migongo yao, na hawakuyajali wakaficha haki na kudhihirisha batili, na wakafanya ujasiri katika maharamisho ya Allah, kwa dharau haki za Allah na haki za viumbe, na wakanunua kwa hilo (kuficha kwao) thamani  ndogo kwa baadhi tu ya vyeo na mali chache, kama ilivyotokea kwa viongozi wao wenye kufuata matamanio yao, wenye kutanguliza matamanio yao kuliko haki, hivyo basi vita vikaenea na udikteta ukadhihiri, wanadamu wakaishi maisha ya kiza juu ya kiza.

Nyoyo zikapata kiza cha ukafiri na ujinga kutokana na hayo. Tabia zikachafuka, maadili, heshima za watu zikaharibiwa na haki mbali mbali ufisadi ukadhihiri katika nchi kavu na baharini, kiasi cha kuwa lau mtu akiangalia kwa akili yenye kufahamu ataona kuwa wanadamu (wakati ule) walikuwa katika hali ya mauti (Sakarati ya Mauti) na kuwa mwisho wao umekaribia, Allah hakuwataka kuleta maslahi makubwa ya utume ambayo itaondoa tatizo lililopo na kuwapelekea watu katika uongofu ili imuongoze mwanadamu njia yake na kumuongoza katika njia ya sawa…

**Tukio tukufu.**

"Tukio moja tu ni miongoni mwa matukio yenye faida zaidi katika historia ya mwanadamu nalo si jingine bali ni kudhihiri kwa Uislamu."

**George Sarton**

Mhadhiri katika Vyuo Vikuu vya Washington na Havard.

Hivyo basi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) katikati ya janga hili lenye kiza katika maisha ya mwanadamu, Allah alimchagua Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ili awe:

Na akamtuma pamoja naye nuru inayoongoza ambayo inamuokoa mwanadamu dhidi ya upotofu na mashaka yake, hadi Allah alipokamilisha dini hii kwa wanadamu na akatimiza neema yake kwa ukamilifu wake, na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akafanya jihadi ili aweze kufikia kwenye haki kwa walimwengu wote: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote} [21:107],

Kiasi cha kuonja njia ya furaha, nae (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) katika jihadi yake yote hakuwa anataka chochote katika starehe za dunia, wala hakutaka ujira kwa watu, Allah amesema: {Sema (Ewe Mtume):Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.} [38:86],

Bali Mola wake alimpa khiyari baina ya kuwa Mtume kwa sura ya malaika au Mtume kwa sura ya mwanadamu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akachagua kuwa mja Rasuli. Ikawa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni mwanadamu anayeishi kama wanadamu wengine, anasikia njaa kama wanavyosikia maswahaba zake, anaumia na kupata majeraha kama wanavyojeruhiwa, na kufanyakazi pamoja nao, na anajifakharisha kuwa ni mja wa Allah, hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anapotaka kumkirimu humsifu kwa uja, "Allah amesema: {Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, ambaye amemteremshia mja wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo.} [18:1],



**Habari ya Ajabu Zaidi.**

"Habari ya kuibuka kwa Uislamu lilikaribia kuwa habari ya ajabu zaidi ambayo historia ya mwanadamu imeandika, kudhihiri kwa Uislamu katika Ummah ambao kabla ya wakati huo ulikuwa hauna utulivu na nchi ilikuwa imeparaganyika. Haikupita muda wa miongo kumi ya kudhihiri kwake Uislamu ulikuwa umeshasambaa nusu ya Ulimwengu ikivunja falme kubwa na kuzitupilia mbali, na kubomoa dini za kale ambazo zimepita zama na vizazi, na hivyo kubadilisha nafsi za umma nyingi na kujenga Ulimwengu mpya wenye nguzo imara nayo ni Ulimwengu wa Uislamu."

**Lothrop Stoddard**

Mwandishi wa Kimarekani





Bali alikuwa akitahadharisha watu kuvuka mipaka na kutoa zaidi ya haki yake, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam): "Msinikweze kama Wakristo walivyomkweza Ibn Maryam, bali mimi ni mja, basi semeni mja wa Allah na Mtume wake." (Bukhari).

Na kila mwenye kumuona na akamjua atajua ukweli wake na akasoma sira yake atashangazwa

## Rehema kwa Walimwengu.

"Maisha ya mfano wa Muhammad. Na nguvu kama nguvu za kuchunguza na kufikiri kwake mambo, jihadi yake, na msimamo wake wa kuondosha upotofu uliokuwa katika Ummah wake na ujahilia wa watu wake na ukali wake wa kupambana na washirikina kunyanyua neno la Mola wake na kufungamana na ujasiri wake katika kuthibitisha nguzo za dini ya Kiislamu. Yote hayo ni dalili kuwa hakukusudia udanganyifu au kuishi katika batili; alikuwa ni mwanafalsafa, khatibu, Mtume, mweka sheria, mwenye kumuongoza binadamu kwenye akili, mwanzilishi wa dini isiyokuwa na udanganyifu. Yeye ni muanzilishi dola ishirini ulimwenguni, na mfunguzi wa nchi ya Kiroho mbinguni. Ni nani aliyepata ukubwa wa Uislamu kama alivyopata yeye!!

**Lamartine**

Mshairi wa Kifaransa.

na tabia yake (Swala Llahu ‘alayhi wasalaam), kwa nini isiwe hivyo wakati maadui zake walimshuhudia kabla ya marafiki, na makafiri kabla ya Waislamu! Inatosha uthibitisho wa Mola wake aliposema:

{Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Bali inatosha kuwa Allah (Subhaanahu wa Ta’ala) alimchagua awe mwisho wa Mitume na manabii, na alipomaliza jukumu lake Allah (Subhaanahu wa Ta’ala) alimfisha, lakini ujumbe wake ukaendelea kubaki hadi Siku ya Malipo.



**Katika wakuu wa watu (Miongoni mwa watu mashuhuri).**

“Muhammad alikuwa ni mtu wa pekee katika historia aliyefanikiwa kwa njia bora zaidi katika viwango vyote vya kidini na kidunia. Kwa hakika mkusanyiko (muunganiko) huu wa pekee ambao hauna mfano kwa ajili ya taathiri ya kidini na kidunia pamoja, linamfanya kuwa mtu mwenye haiba tukufu zaidi yenye taathira katika historia ya mwanadamu.”

**Michael Hart**

Mwandishi wa Kimarekani.

## MIONGONI MWA DALILI ZA UTUME WAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)

Kuwa amelingania kumuabudu Allah Ta'ala peke yake na kuacha kuabudu wasiokuwa yeye, akiafikiana katika hilo na Mitume wote, na atakayelinganisha baina ya aliyokuja nayo Musa, Issa ('Alayhi salaam) na yale aliyokuja nayo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) miongoni mwa akida sahihi na sheria na hukumu mbali mbali na elimu mbali mbali zenye manufaa atajua na kufahamu kuwa yote hayo yanatoka katika kijaruba kimoja nayo ni taa ya utume.



### Hamkanushi isipokuwa ni Mpingaji

"Muhammad ni Mtume wa kweli kwa maana halisi ya neno. Kamwe hatuwezi kukana kuwa Muhammad ndio kiongozi mwenye kuelekeza kwenye njia ya kuokoka."

**Hans Kung**
Mwanazuoni wa kidini wa Switzerland

Kuwa alidhihirisha miujiza na alama mbali mbali ambazo hazidhihirishwi ila na Mitume ya Allah; kwani Sunnah ya Allah Ta'ala imepita katika mikono ya Manabii waliopita imevunja ada (mazoea) ili iwe ni miujiza kwao, na dalili ya ukweli wao, na nia ya kusimamisha hoja kwa kaumu yao, na miujiza ya kila Mitume ilikuja kwa jinsi ambayo kaumu ya mtume yule ilivyopiga maendeleo katika jambo fulani. Hivyo basi muujiza wa Musa ('Alayhi salaam) ukanasibiana na jinsi kaumu yake ilivyopiga hatua katika fani maalumu; nayo ni fani ya uchawi, Allah kwa miujiza aliompa Musa akabatilisha uchawi wao, na wakashindwa kushindana na Musa katika hilo pamoja na werevu mkubwa na uhodari wa hali ya juu waliokuwa nao katika aina mbalimbali za uchawi. Kaumu ya Issa ('Alahyi Salaam) waliiga maendeleo makubwa katika fani ya utabibu na madawa, Allah akawaponya katika mikono ya Issa ('Alahyi Salaam) katika maradhi yaliyoshindikana

kutibiwa kiasi cha kuwa Allah akawafufua wafu katika mikono ya Issa ('Alahyi Salaam).

Miujiza yote hii ilikuwa ni ya kihisia (yaani yenye kuonekana), imefungamana na mahali na zama maalum, haina sifa ya kilimwengu na kudumu, miongoni mwa miujiza ya Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni kama miujiza ile ya kihisia; miongoni mwa miujiza hiyo ni:

Kububujika maji kutoka katika vidole vya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam).

Chakula kidogo kukifanya kingi kiasi cha kula yeye pamoja na Waislamu wengine walio nae, na kubakia.

Kufanya maji kuwa mengi kiasi cha kunywa jeshi zima na kutawadha.

Gogo kumlilia alipoacha kulitumia katika mimbari.

Jiwe kumsalimu alipokuwa Makkah.

Mti kumnyenyekea yeye.

Changarawe kusabahi katika kiganja chake.

Kuponya magonjwa kwa uwezo wa Allah, na mengineyo,

Qur-aan imerikodi moja katika miujuza ile muujiza wa Israa na Miiraji; Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alipopelekwa Israa kutoka msikiti wa Masjid Al-Haram Makkah kuelekea Al-Masjidil Aqswaa, kisha akapaishwa Mii'raj kutoka katika msikiti wa Aqswa hadi mbingu ya saba, Allah Ta'ala amesema:



## Maneno ya Mwenyezi Mungu.

Nilipomaliza kusoma Qur-aan nikajawa na hisia kuwa hii ndio haki ambayo inakusanya majibu toshelevu kuhusu maumbile na mengineyo. Kadhalika hutupa matukio kwa njia ya mantiki ambayo tunaona yakigongana na vitabu vingine vya dini. Ama Qur-aan inayazungumzia kwa njia nzuri yenye kupendeza ambayo haiachi fursa ya mtu kutia shaka kuwa huu ndio ukweli, na ya kuwa maneno haya bila ya shaka ni ya Mwenyezi Mungu.

**Deborah Potter**

Mwandishi wa Kimarekani





## Hazifanani.

"Hakuna mfano wa Uislamu, dini ambayo imetukuza Manabii na Mitume ambao walikuja kabla ya Mtume Mwarabu. Dini hii imewataka waumini wake kuwatukuza watu hawa na kuwaamini. Hakuna dini iliyo sawa na Uislamu katika kuheshimu dini zingine zilizoteremka ambazo zilitangulia katika kuteremka na Wahyi."

**Nassry Salhab**

Mwanafasihi wa Kilebanoni.



{SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.} [17:1].

Vivyo hivyo muujiza wa kupasuka kwa mwezi; ambapo Allah Ta'ala amesema: {Saa imekaribia, na mwezi umepasuka!} [54:1],

Na hii ilitokea wakati Makafiri walipomtaka Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) athibitishe ukweli wake kwa muujiza uliokuwa wazi kabisa, na wakaainisha wazi awapasulie mwezi, na kuahidi kuwa baada ya hapo wataamini, siku hiyo ya tukio ilikuwa ni siku ya mwezi kamili (Badri), yaani: usiku wa siku ya kumi na nne ya mwezi; ambao mwezi unakuwa kwa ukamilifu wake na kwa uwazi zaidi..

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akamuomba Mola wake ampe walichokiomba; mwezi ukapasuka mara mbili: nusu ikawa juu ya mlima wa Saffa na nusu nyingine juu ya Jabali Qayqu'aan inayoelekeana nayo, baada ya kupatikana kwa muujiza huu mkubwa washirikina wa Kikureishi hawakuamini, bali waliuzingatia kuwa ni uchawi, na huu ndio mwendo wa wapingaji wa dini ya Allah.



### Kwa Ulimi Bainifu wa Kiarabu

"Aya ambazo Muhammad amerudia kuzitaja katika sura hizi tukufu zimeacha mbali nyuma yake kauli za wanadamu fasaha zaidi kama ambavyo inawezekana kuzileta kupitia maandiko yaliyowekwa ambayo yametufikia."

**Régis Blachère**

Mustashrik wa Kifaransa.

Ni kawaida ya wapingaji pindi haki inapobomoa utawala wao na nuru ya Allah inapofunika upotofu wao, hapo hufanya vitimbi na kusimama mbele yake, ima kwa kupotosha misingi yake au kugeuza hakika zenyewe, kwa dhana ya kuwa hayo yatatosha kumaliza na kuangamiza ukweli wenyewe, Allah amesema: {Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu uchawi tu unazidi kuendelea. Na wamekanusha na wamefuata matamanio yao. Na kila jambo ni lenye kuthibiti.} [68:2-3].

Qur-aan: Ni muujiza mkubwa zaidi, ni wenye kubaki katika karne zote na dahari, nao ni muujiza wa kimaana na kiakili na alama miongoni mwa alama za utume; kwa sababu ni kitabu fasaha zaidi, Allah amemteremshia (Mtume) Ummiyyi (asiyesoma yaliyoandikwa), ikawa ni changamoto kwa watu wenye ufasaha zaidi walete sura moja mfano wa Qur-aan.

Muujiza uliopo kwenye Qur-aan na changamoto yake na hakuna yoyote mwenye kukanusha hayo isipokuwa mwenye kiburi.

Kwa hiyo inashinda kwa ufasaha wake, balagha yake, umbuji, utaratibu na mpangilio wake, na yaliyomo ndani yake miongoni mwa habari zilizopita na zinazokuja,



kadhalika sheria na hukumu mbali mbali na maadili ya juu zaidi uongofu, nuru na baraka.

Kama ambavyo miujiza ya kisayansi inayovumbuliwa kila siku inakubaliana na habari za wahyi madamu ni hakika za kisayansi ulimwenguni, ambazo hazikuwa zikifahamika hapo kabla zote hizo ni uthibitisho bayana wa ukweli wa utume wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), kama ambavyo sayansi leo hii ilivyovumbua hatua mbali mbali (tofauti) anazopitia kichanga anapokuwa tumboni kwa mama yake na kuwepo kwa kizuizi cha maji baina ya maji tamu na maji chumvi baharini na mifano mingine kama hiyo.

Hata hivyo uthibitisho mkubwa zaidi za kuwa kwake kutoka kwa Allah ni kubakia kwake ikiwa imehifadhiwa zaidi ya karne kumi na nne bila ya kupotoshwa, au kubadilishwa, wala hachoki msomaji wake hata akikariri mara nyingi kwa kuisoma, Allah amesema: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9].

Bali Qur-aan yenyewe imehifadhi akida (itikadi) sahihi ikiwa na sheria kamili ndani yake, na ikasimamisha Umma bora kabisa, hapa inatudhihirikia sisi kuwa muujiza wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) umekuwa bora tofauti na miujiza ya ndugu zake manabii na Mitume (Swala Llahu



**Qur-aan na Sayansi bega kwa bega.**

"Nilifanya utafiti kuhusu Qur-aan Tukufu bila ya kuwa na fikra yake yoyote hapo kabla, na bila upendeleo. Lengo ni kutafuta kiwango cha maafikiano kati ya Qur-aan na kinachopatikana katikaelimu leo hii. Nilichokipata ni kuwa Qur-aan haina aya au andiko linaloweza kukosolewa kwa upande wa elimu katika zama hizi."

**Maurice Bucaille**

Maurice Bucaille



**Hayo ni Maneno ya Mwenyezi Mungu.**

"Mimi sina shaka japo mara moja katika ujumbe wa Muhammad na ninaamini kuwa yeye ni Mtume wa mwisho. Ametumwa kwa watu wote na ujumbe wake umekuja kuhitimisha Wahyi uliokuja katika Torati na Injili. Dalili nzuri kabisa katika hilo ni Qur-aan yenye miujiza. Mimi napinga fikra za Pascal mwanazuoni wa Ulaya mwenye chuki kubwa ya Uislamu na Waislamu isipokuwa fikra moja tu: nayo ni kauli yake: Qur-aan sio katika utunzi wa Muhammad kama ambavyo sio katika utunzi wa Mathayo."

**F. Motague**

Mwanafikra na Mvumbuzi wa Kifaransa.

'alayhi wasallam) waliotangulia kwa kulinganisha ukubwa wa miujiza ile, pia miujiza ya Mtume Muhammad ni ya watu wote ulimwenguni na wa zama zote na ni muujiza utakao dumu milele.

Changamoto inaendelea kusimama dhidi ya wote wataendelea kushindwa kuleta mfano wa Qur-aan hii, Allah amesema:

{Sema: Wangeli kusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao.} [17:88].

Kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alitabiri matukio mbalimbali ulimwenguni na yalitokea kama alivyosema; kama vile Fathi (ufunguzi) ya Shaam, Iraq na Constantinople (uturuki). Hali kadhalika ameelezea kuhusu Ummah mbali mbali zilizopita na hali zao pamoja na manabii na mitume wao, kuanzia Adam ('Alayhi salaam), Nuuh, Ibrahim, Musa na Issa ('Alayhi salaam), kama ambavyo alitabiri matukio ya siku za usoni; na yakatokea kama alivyotabiri na miongoni mwa hayo ni pale Wafursi walipowashinda Warumi, Allah akaeleza kuwa baada ya miaka michache Warumi watawashinda Wafursi, Allah amesema: {Alif Lam Mim (A.L.M.) Warumi wameshindwa, Katika nchi iliyo karibu. Nao baada ya kushindwa kwao watashinda Katika miaka michache. Amri ni ya Mwenyezi Mungu kabla yake na baada yake. Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui. Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.} [30:1-7],

Na tukio hilo likatokea kama alivyolielezea Allah (Subhaanahu wa Ta'ala).

Manabii ('Alayhi salaam) wametabiri kuja kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kabla ya kuja kwake kwa dahari nyingi wakatoa wasifu wa kutumwa kwake, mji na umma na mataifa mbali mbali na wafalme kumnyenyekea yeye na umma wake na wakataja kuenea kwa dini yake.

Kuwa yeye ni mwisho wa Mitume, na kama asingetumwa basi utabiri wao ungekuwa batili.

Ukweli wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuthibiti jambo lake katika Taurati na Injili, na baadhi ya watu katika Ahlul kitabu wakati wa kutumwa kwake ambao kasumba haikuwapofusha (kufanya hivyo); kama vile mtawa Bahira, bwana Waraqa bin Nawfal, sahaba Salman Al-Faarisy, aliyekuwa mwanazuoni wa kiyahudi kabla hajasilimu Abdallah bin Salaam na Zaid bin Sa'atah.

Ushindi wake kwa Ummah mbali mbali aliopigana nao ni dalili na alama miongoni mwa alama za utume wake; kwani ni muhali kwa mtu kujidai kuwa ametumwa na Mwenyezi Mungu (nae ni muongo) kisha baada ya hapo Allah ampe ushindi na kumuwezesha kuwashinda maadui, da'wah yake kuenea na kuongezeka kwa wafuasi wake, hilo halitokei ila katika mikono ya Mtume Mkweli.

Ibada yake Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), ukweli wake, historia yake nzuri, mwendo wake, sheria yake na tabia yake njema, kwani aliyemtengeneza katika adabu hizo ni Mola wake: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],



**Ni tengenezo la Mwenyezi Mungu.**

"Katika zama ambazo nchi nyingi zilianguka, nchi ambazo hapo kabla zilikuwa sehemu ya utawala wa –Ufalme wa kale wa Diocletian. Ghafla katika moyo wa majangwa ya Arabia aliibuka mtesi (utesi). Ufalme ule uliochoka ukawa unafuatilia mtesi Yule kama kwamba ni ufalme mpya ambao ulikuwa unaibukia Magharibi. Uadui huu ulikuwa unapanuka siku hadi siku machoni mwa watu. Na ulinzi wa Mwenyezi Mungu ndio ambao daima ulikuwa ukiwaongoza askari wale wakweli na waaminifu kuelekea kwenye jihadi na ushindi mkubwa. Ushindi ule ulipelekea kufunguliwa kwa Syria na Misri, na baada ya hapo ufalme wa Wasasani wakaingia katika mazungumzo na Wakonstantini wakitishiwa na muelekeo ule (wa ushindi wa Waislamu)."

**Aldo Mieli**

Mustashrik wa Kifaransa.

Kwani sifa hizi tukufu hazikusanyiki isipokuwa kwa Nabii wa kweli.

Njia ya upokeaji wa habari ya Tawaatur ambayo utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) umenukuliwa pamoja na miujiza yake, mwenye kuangalia kwa makini hali za manabii mbali mbali na kusoma historia zao; atafahamu ufahamu wa yakini kuwa hakuna njia iliyothibitisha utume wa Nabii yoyote ila njia hiyo vile vile imethibitisha utume wa Nabii Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam).

Ukiangalia namna utume wa Musa na Issa ('Alayhima salaam) ulivyonukuliwa, utafahamu kuwa imenukuliwa kwa njia ya Tawaatur, na ndio Tawaatur iliyonukuu utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni tukufu zaidi na yenye kuaminiwa zaidi, kadhalika Tawaatur iliyotumika kunukuu miujiza na alama mbali mbali ni zenye kufanana, bali ya Muhammad ni kubwa zaidi na ni zama za karibuni zaidi; kwa sababu miujiza yake ilikuwa ni mingi zaidi, bali muujiza ulio mkubwa zaidi ni hii Qur-aan ambayo inaendelea kunukuliwa na kupokewa kwa njia za tawaatur kwa njia ya sauti na maandiko.

Kutosoma kwake kilichoandikwa na kutoandika kwake ni dalili ya miujiza yake, Allah alimtumia Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akiwa hasomi na kuandika na huu ni uthibitisho kuwa Qur-aan tukufu imeshushwa kwake na Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na ni dalili





kubwa sana na haswa kwa kuwa yeye ameishi pamoja na watu wake miaka mingi sana na lau angekuwa anajua kusoma yaliyoandikwa washirikina wangedai kuwa alichokuja nacho ni katika uvumbuzi wake na katika fikra zake. Allah amesema: {Na namna hivi tumekuteremshia Kitabu (cha Qur'ani). Basi wale tulio wapa Kitabu (cha Biblia) wataiamini (Qur'ani), na miongoni mwa hawa (washirikina) wapo watakao iamini. Na hawazikatai Ishara zetu isipo kuwa makafiri. Na wewe hukuwa kabla yake unasoma kitabu chochote, wala hukukiandika kwa mkono wako wa kulia. Ingeli kuwa hivyo wangeli fanya shaka wavunjifu.} [29:47-48], Kama inavyothibitisha kuwa aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ni kutoka kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na sio kutoka kwake mwenyewe (yeye Muhammad), Allah amesema: {Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye watu wasio jua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri.} [62:2]

Katika wasifu wa Mtume Umiyyi ambaye anawasomea wasiojua kusoma aya za Allah, yaani Wahyi



wake, na kuwatakasa na kuwafundisha kitabu, yaani anawakaririsha hicho, kama ambavyo Mitume walivyokuwa wanawatamkisha Ummah kitabu kwa kuandika na kuwaelimisha hekima ambayo Mitume iliyotangulia imefundisha Ummah zao. Katika wasifu wote huu kuna changamoto kwa muujiza wa Ummiyyi (kutosoma yaliyoandikwa) katika Mtume huyu (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), pamoja na kuwa kwake Ummiyyi ameletea Ummah wake faida nyingi ambayo Mitume iliyosoma imewapelekea Ummah zao, hakuna upungufu wowote, hivyo Ummiyyi wenyewe umeibuka kuwa ni muujiza umempatisha sahibu yake yaliyo bora zaidi kuliko waliyoyapa mitume wenye kuandika kama vile Musa ('Alayhi salaam).



**Tabia za Utume.**

"Kwa hakika mimi nampenda Muhammad: Sababu ni ile tabia yake safi aliyonayo na mawazo na fikra zake. Kwa hakika mtoto huyu wa majangwani alikuwa ni mwanamme mwenye rai huru: Hujitegemea mwenyewe tu wala hajidai yasiyokuwepo, hakuwa mwenye kiburi!! Hata hivyo hakuwa dhalili, akisimama na nguo zake zenye viraka kama vile alivyompatia Mola wake na kama alivyotaka mwenyewe. Huzungumza na wafalme wa Kirumi na wa Kiajemi kwa maneno yake yenye kutetemesha anawaelekeza maisha haya na maisha ya akhera. Alikuwa anajua uwezo wa Nafsi yake, alikuwa ni mtu mwenye kupitisha azma yake, hacheleweshi kazi ya leo hadi kesho."

**Thomas Carlyle**

Mwandishi na Mwanahistoria wa Scotland.



# UTUME WA MWISHO

Hekima ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) imepelekea kumtuma Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kwa ujumbe wake kwa watu wote wa ardhi, yenye kunasibiana na zama na mahala pote, Allah amesema: {Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji. Lakini watu wengi hawajui.} [34:28],

Na akauhifadhi (ujumbe huo) kutokana na kubadilishwa na kugeuzwa; ili ujumbe wake ubakie hai watu wanaishi nao, ikaepushwa na upotofu na kubadilishwa na kwa ajili hiyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akaufanya kuwa ni ujumbe wa mwisho, na akamhusisha nao Muhammad, kwa sababu yeye ndie mtume wa mwisho, hakuna nabii baada yake; kwa kuwa Allah amekamilisha kwake ujumbe (utume), na akahitimisha kwake sheria na akatimiza jengo lake.



## Dini ni Moja.

"Dini ya Manabii wote ilikuwa ni moja tu: Wao ni wamoja katika mwendo wao tokea Adam hadi Muhammad, vilishuka vitabu vitatu toka mbinguni navyo ni: Zaburi, Torati na Qur-aan. Mfano wa Qur-aan kwa torati ni mfano wa torati kwa Zaburi. Muhammad kwa mtazamo wa Issa ni kama vile Issa kwa mtazamo wa Mussa, lakini jambo la muhimu kulifahamu ni kuwa Qur-aan ni kitabu cha mwisho kutoka mbinguni imeteremka kwa watu na mwenyewe (Muhammad) ni Mtume wa mwisho. Hakuna tena kitabu baada ya Qur-aan wala Nabii baada ya Muhammad."

**Henri de Castriesry**

Luteni wa zamani katika jeshi la Ufaransa.



### Kitabu cha Mwisho Kuteremka.

"Hapo kabla Torati ndio iliokuwa muongozo kwa watu na msingi wa tabia zao. Hadi alipodhihiri masihi Wakristo walifuata mafundisho ya Injili. Kisha ikaja Qur-aan na kuchukua nafasi zao. Qur-aan ilikuwa ni pana zaidi na yenye maelezo zaidi kuliko vitabu viwili vilivyoitangulia kama Qur-aan ilivyoweza kusahihisha uzushi yaliyoingizwa kwenye vitabu vilivyotangulia. Qur-aan imekusanya kila kitu, imekusanya sheria na kanuni zote. Kwani hicho ndicho kitabu cha mwisho kutoka mbinguni."

**Washington Irving**

Mustashrik wa Kimarekani.

Kwa ajili hiyo Allah amekifanya kitabu alichokuja nacho Muhammad kuwa ni mtawala juu ya vitabu vilivyotangulia na kinachovifuta, kama vile ambavyo sheria aliyokuja nayo Muhammad (Swala Llahu'alayhi wasallam) kufuta sheria zilizomo kwenye vitabu vilivyotangulia, Allah mwenyewe amedhamini kuhifadhi ujumbe wake; na hivyo ikawa inanukuliwa na kupokewa hali ya kuwa ni tawaatur; na hivyo ndivyo ilivyonukuliwa na kupokewa Qur-aan ikiwa ni tawaatur kwa sauti (jinsi isomavyo) na kwa kuandikwa jinsi iandikwavyo, kadhalika sheria ya dini hii na ibada zake zimenukuliwa jinsi ilivyokuwa ikitendwa kunukuliwa kwa njia ya tawaatur na sunnah zake na hukumu zake mbali mbali.

Mwenye kuangalia katika vitabu mbali mbali vilivyonukuliwa Sira na Sunnah za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ataona kuwa sahaba zake

(Radhiya LLahu 'anhum) waliweza kuwahifadhia watu hali za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), maneno yake yote, na matendo yake, na hivyo basi wakanukuu ibada zake kwa Mola wake na dhikri zake, istighfaar, jihadi zake, ukarimu wake, ushujaa wake, namna alivyokuwa akiishi na sahaba zake na wanaomtembelea, kama walivyonukuu furaha yake ilivyokuwa, huzuni yake, safari zake na kutosafiri kwake, wasifu wa kula na kunywa kwake, na kuvaa kwake, kuamka na kulala kwake,utakapojua hilo utayakinisha kuwa dini hii imehifadhiwa kwa Allah kuuhifadhi,na wakati huo utajua kuwa yeye ni hitimisho la mitume na manabii; Allah amesema: {Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [33:40].



## Mwalimu wa Wanadamu

"Mwenendo wa Mtume wa Waarabu umechukua (umeshika) akili za wafuasiwake; na haiba yake ikapanda kwao juu zaidi. Waliamini ujumbe wake kwa imani ambayo imewafanya wakubali Wahyi ulivyokuwa ukiteremka kwake. Kama ambavyo matendo yake (kama yalivyorekodiwa na Sunnah) ilikuwa ni chanzo cha kanuni. Kanuni ambazo haziishi katika kupanga maisha ya Kiislamu peke yake, bali yaliambatana vile vile na mahusiano ya Waislamu Wafunguzi (kwa nchi nyingi) na raia zao na wasio Waislamu."

**Arnold J. Toynbee**

Mwanahistoria wa Uingereza.

## Mwisho wa Utume

“Mimi ni mmoja miongoni mwa waliofurahishwa na Nabii Muhammad aliyechaguliwa na Mwenyezi Mungu mmoja, ili ujumbe wa mwisho uwe juu ya mikono yake, na pia yeye awe Mtume wa mwisho.”

**Tolstoy**
Mwanafasihi wa Kirusi.





## Muabuduni Mwenyezi Mungu.

“Muhammad alikuwa Mtume wa mwisho Mtukufu ambae ametumwa na Mwenyezi Mungu ili awalinganie watu katika kumuabudu Mwenyezi Mungu.”

**Washington Irving**
Mustashrik wa Kimarekani





## REHEMA KWA WALIMWENGU

Allah amemtuma Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kuwa rehma kwa walimwengu wote wanaume kwa wanawake, watoto kwa wakubwa, bali Allah amemtuma kuwa rehema hata kwa wasiomuamini, na rehema hii inaonekana wazi katika misimamo ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) maisha yake yote, na mingi inaonekana alipokuwa akilingania watu wake (akiwahurumia) walimkadhibisha na kumfukuza kutoka katika mji wake Makkah na kujaribu kumuua, Allah akawa ndiye anayemtosha kwa kila kitu akawarejeshea vitimbwi vyao Allah amesema: {Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.} [8:30]

Na yote hayo hayakumzidishia isipokuwa rehema, huruma na kujali zaidi katika kuwaongoa, Allah Ta'ala amesema: {Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.} [9:128],

### Uislamu wa Kilimwengu.

"Kwa hakika aya za Qur-aan ambazo zinaashiria kwenye Uislamu wa Ulimwengu kwa wasifu wake kuwa ni dini ambayo Mwenyezi Mungu amemteremshia Nabii wake kuwa (Rehema kwa Walimwengu): Huo ni mwito wa moja kwa moja kwa Ulimwengu wote. Hii ni dalili ya wazi kuwa Mtume alijua kwa yakini yote kuwa ujumbe wake umekadiriwa kuvuka mipaka ya Ummah wa Kiarabu, na kuwa ni juu yake kufikisha neno jipya kwa watu wanaonasibika na jinsi tofauti wenye kuzungumza lugha tofauti."

**Laura VecciaVaglieri**

Mustashrik wa Italia



Na baada ya kuwashinda katika siku ya ukombozi wa Makkah aliwasamehe, na Allah alipomtuma Malaika ili awabamize Makafiri kwa milima miwili mikubwa ili waangamie, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alisema: "Bali nitasubiri huenda Allah akatoa ndani ya migongo yao wenye kumuabudu Allah peke yake"



Allah Ta'ala amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Yeye ni rehema kwa Walimwengu, kwa watu wote pamoja na tofauti walizonazo za rangi zao, lugha zao, mitazamo yao, fikra zao, itikadi zao na sehemu zao.

Rehema hii haijaishia kwa wanadamu tu, bali imefika hadi kwenye wanyama na vitu visivyo na uhai. Kwa mfano yule ngamia wa mmoja wa wakazi wa Madina ambaye aliadhibiwa na mwenye ngamia akawa anamtesa kwa njaa kali, kwa hiyo moyo wa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ukamhurumia na kuamuru mwenye ngamia kumfanyia wema ngamia wake na kutomtumikisha zaidi ya uwezo wake.

Mara moja Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alipoona mtu amechukua vitoto vya njiwa alimhurumia njiwa yule na

kuamrisha kurejeshewa vitoto vyake, naye Mtume ndie aliyesema: «Na mnapochinja chinjeni vizuri.» (Muslim).

Kama ambavyo huruma ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) ilivyoenea kwa vitu visivyo na roho, alilihurumia lile gogo ambalo lilisikitika na kulia kwa kuachana na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) hivyo akalihurumia na akateremka (kutoka mimbarini) na kukikumbatia hadi kiliponyamaza na kutulia.

Huruma yake haikuwa kwenye mitazamo na matukio peke yake, bali ni amri, sheria, mfumo na tabia njema ambayo ameifanya kwa ajili ya watu.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) amenukuliwa akisema katika kuhamasisha huruma, wema na ulaini kwa watu, na akaonya na kutahadharisha atakayefanya ugumu juu yao, akasema: «Ewe Mola wangu atakayetawalia jambo katika Ummah wangu akawafanyia watu ugumu, mfanyie ugumu, na atakayetawalia jambo katika umma wangu akawahurumia basi mhurumie.» (Muslim).

Hivyo basi rehema (huruma) ni tabia njema katika tabia njema za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam), na msingi muhimu katika dini ya Kiislamu ni kuwa dini hii ni ya huruma na amani.

## Ni Rehema iliyozawadiwa watu

"Maisha ya Kihistoria ya Muhammad hayawezi kupata wasifu mzuri zaidi ya ule alioueleza Mwenyezi Mungu pale aliposema: "Na hatukukutuma isipokuwa rehema kwa Walimwengu." Yatima Mtukufu ametoa rehani Nafsi yake kuwa yeye ni rehema kubwa kwa kila mnyonge na kila mhitaji. Muhammad alikuwa rehema kweli ya yatima, wapita njia (wasafiri), waliopatwa na maafa, fukara wote na wafanyakazi wa kima cha chini wenye tabu na usumbufu."

**Jan Lake**

Mustashrik wa Hispania



# FURAHA YA MWANADAMU KWA KUTUMWA KWAKE (Swala Llahu 'alayhi wasalaam)



**Mwenye kuwatoa wanadamu kutoka kwenye kiza hadi kwenye nuru.**

"Nabii Muhammad aliwafikisha viumbe kwenye kiwango cha juu zaidi cha furaha kwa haraka sana. Na atakayeangalia kwa jicho la busara na uoni wa kina katika hali za wanadamu kabla ya hapo na upotofu waliokuwa nao, na akaangalia hali zao baada ya hapo na yaliyowakuta katika zama zao katika maendeleo makubwa utaona tofauti kubwa kati ya hali mbili hizo kama ilivyo kati ya mbingu na ardhi."

**Abdullah Quilliam**
*Mwanafikra wa Uingereza*

Utume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) umekuja kwa hiyo watu wakaongoka kwa baraka za utume wa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam), na ubainifu na uongofu, aliyokuja nayo (hidaya). Uongofu ambao uko wazi kuliko maelezo ya wanaousifia na kuwa juu ya maarifa ya wajuzi.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuja na elimu yenye manufaa, matendo mema, tabia tukufu kabisa, mwenendo ulionyooka, ambao lau zingekusanyika hekima zote na elimu za watu wote na Ummah zote na matendo yake kulinganisha na hekima aliyotumwa nayo Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) basi zingetofautiana na tofauti kubwa, kuhimidiwa ni kama apendavyo mola wetu na kuridhia.

Kwa upande wa akida; shirki ilikuwa imeenea kwa wanadamu na kumuabudu asiyekuwa Allah, kutokana na watu waliopewa kitabu kutoka mbinguni ambavyo vilipotoshwa.

Kwa hiyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akaja na tawhidi halisi na kumuabudu Allah peke yake

na kutomshirikisha na chochote, na kuwatoa watu katika kuabudu watu na kuelekea kumuabudu Mola wa waja, hivyo kutakasa nafsi zao kwa tawhidi na kuondosha uchafu wa ushirikina na uchafu wa kuabudu asiyekuwa Allah. Hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) akamtuma kwa yale aliyowatuma nayo Mitume kabla yake, Allah amesema: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.} [21:25],

Na akasema Allah vilevile: {Na Mungu wenu ni Mungu mmoja tu, hapana mungu ila Yeye. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.} [2:163].

Kwa upande wa kijamii, Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alitumwa zama ambazo dhuluma, udikteta na kuabudiwa watu kulikuwa kumetawala, utabaka unaochukiza ulikuwa umewagawa wanadamu katika tabaka nyingi, kila tabaka linatumikisha tabaka lingine na yanadhulumiana, Mtume Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akaja na kuwafanya watu wote kuwa sawa, Muarabu kwa Muajemi, mweupe kwa mweusi, hakuna mbora ila kwa ucha-Mungu na amali njema, Allah amesema: {…Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi...} [49:13]

Na akaamrisha uadilifu, wema, kushikamana kijamii na kukataza dhulma, munkari na uadui, Allah amesema: {Hakika Mwenyezi Mungu anaamrisha kufanya uadilifu, na hisani, na kuwapa jamaa; na anakataza uchafu, na uovu, na dhulma. Anakuwaidhini ili mpate kukumbuka.} [16:90]



**Dini ya watu wote.**

"Aya mbili: "Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu…." (3:19) na "Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji" (34:28) zimeacha athari kubwa sana Katika nafsi yangu: Kwani ndani yake kuna dalili ya ile sifa ya kielmu ambao Uislamu umepambauka nao mbali na zile sifa unazosifika nazo Uislamu za nidhamu na sheria nyingine na ubainifu wake kamili wa ukweli wa Nabii Issa. Je, kuna ukweli wenye nguvu zaidi kuliko mafundisho yale huru ambayo yanatuusia kuheshimu kila walichokuja nacho Mitume na manabii?! Hapana shaka yoyote kuwa dini ya Kiislamu ni dini ya haki, dini ya kweli na dini yenye hoja na dalili."

**Wagner**

Mtafiti wa Kidachi (Uholanzi).

Bali akahifadhi haki za watu, na kukataza kundi moja kudharau kundi lingine, Allah amesema: {Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao. Wala msivunjiane hishima, wala msiitane kwa majina ya kejeli. Ni uovu kutumia jina baya baada ya kwisha amini. Na wasio tubu, hao ndio wenye kudhulumu.} [49:11].

Upande wa tabia; Allah amemtuma Mtume wake na tabia za watu zilikuwa duni, chafu na mbaya sana, hakukuwa na maadili mema wala tabia njema, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akaja kuwarudisha watu kwenye maadili mema na adabu tukufu; ili maisha yao yafurahi kwa miamala mizuri, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) amesema: "Kwa hakika nimetumwa kutimiza mazuri ya tabia." (Al-Bayhaqi).

Bali Allah amesifu tabia yake kuwa ni tukufu; Allah amesema: {Na hakika wewe una tabia tukufu.} [68:4],

Nae alikuwa ndie kiigizo chema katika tabia na adabu, na mfano mzuri katika kuipa nyongo dunia, Ucha-Mungu na muamala – mzuri na maneno mazuri bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) alikuwa ni kigezo kizuri katika kila kitu kizuri, Allah Ta'ala amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.} [33:21].



**Mafunzo kutoka katika Hijja ya kuaga.**

"Muhammad alihiji Hija ya kuaga kutoka Madina kwenda Makkah kabla ya kifo chake kwa mwaka mmoja. Wakati huo alitoa mawaidha makubwa kwa watu wake. Sentensi ya kwanza tu aliondosha mbele yake yote waliyokuwa nayo Waislamu kama vile unyang'anyi, uizi, kulipiza kisasi, na umwagaji wa damu, na paragrafu ya mwisho alisisitiza usawa kati ya muumini wa Kihebeshi na Khalifa wa Waislamu. Kwa hakika aliweka msingi mkubwa Ulimwenguni kwa ajili ya kuamiliana kwa uadilifu na ukarimu."

**H. G. Wells.**

Mwandishi na Mwanafasihi wa Kiingereza.



Ama mwanamke alikuwa anasumbuka kwa mengi kabla ya Allah kumtuma mtume wake, wakati huo mwanamke akidhalilishwa na hana haki yoyote, watu walitofautiana kuhusu mwanamke; Je, ni mwanadamu au la? Je, ana haki ya kuishi au huuawa na kuzikwa akiwa mdogo?! Watu walikuwa kama vile walivyosifiwa na Allah (Subhaanahu wa Ta'ala): {Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyo bashiriwa! Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni? Tazama uovu wa wanavyo hukumu!} [16:58-59],

Alikuwa ni mdoli tu anachezewa na watu na kustarehesha, akiuzwa na kununuliwa, kiumbe kinachodharauliwa, hivyo Allah hivyo Allah akamtuma Mtume wake kwa ajili ya kumtukuza, kumkirimu mwanamke, Allah Ta'ala amesema:

{Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [30:21],



## Tabia ya Nabii wa Allah Muhammad.

"Muhammad alikuwa ni mtukufu mno na maadili mema, alikuwa mwingi wa haya mwenye hisia kali. Alikuwa ni mwenye ufahamu mkubwa na akili nyingi, mpole na mwenye heshima."

**Abdullah Quilliam**

Mwanafikra wa Uingereza



### Njia ya Ulimwengu.

"Nimesoma vizuri maisha ya Muhammad Mtume wa Uislamu mara nyingi, sikupata ndani yake ila matukufu ya tabia kama kinavyotakiwa kuwa.Ni mara ngapi nimetamani Uislamu kuwa ndio njia ya Ulimwengu."

**Sir George Bernad Shaw**

Mwandishi wa Uingereza.



### Hadhi ya Mwanamke.

"Uislamu umemnyanyua mwanamke katika nchi za Kiarabu, na hivyo ukamaliza desturi ya kuua mabinti na akaweka usawa baina ya mwanaume na mwanamke katika taratibu za kisheria na uhuru wa matumizi ya mali, na akajaalia miongoni mwa haki yake ni kufanya kazi yoyote ya halali. Na kuhifadhi mali na mapato yake, kurithi na uhuru wa kutumia mali yake atakavyo, na hivyo kufuta ada waliokuwa nayo Waarabu katika zama za Ujahilia ya wanawake kurithiwa na baba zao au watoto wao kama vile zinavyorithiwa mali na mizigo, na ukafanya fungu la mirathi ya mwanamke ni nusu ya fungu la mwanaume na akakataza kuozeshwa bila ya matakwa yao."

**Will Durant**

Mwandishi wa Kimarekani

Bali aliamrisha afanyiwe wema kama mama, Allah amesema: {Na Mola wako Mlezi ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema….} [17:23],

Na wema kwake ukatangulizwa kuliko wema wa mwanaume, wakati mmoja mtu alikwenda kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kusema: «Ewe Mtume wa Allah, ni nani mwenye haki zaidi ya kusuhubiana nae? (Mtume) akajibu: "Ni Mama yako", akasema: kisha nani? Akasema: "Mama yako".

Akasema: "kisha nani?" Akasema: "Mama yako". Akasema kisha nani? Akasema: "Baba yako.» (Al-Bukhari).

Kadhalika Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) «ametaka akirimiwe akiwa ni msichana, akasema (Swala Llahu 'alayhi wasalaam): "Aliye na wasichana watatu anawalea, kisha akawahurumia, na kuwatunza, mtu huyu imempasa pepo kabisa amesema: ilisemwa: Ewe Mtume wa Allah, Je, akiwa na wawili (Mtume) akasema: "Na wawili:» (Imepokewa na Ahmad).

Vile vile mwanamke huyo akiwa ni mke ameamrishwa apewe hadhi yake kwa kuunganishwa na wema wake, hivyo Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) akasema: «Mbora wenu ni Mbora wenu kwa familia yake, na mimi ni Mbora wenu kwa familia yangu.» (Imepokewa na Ibn Majah).





**Jeuri na Dhuluma!!**

"Vikao vya Wanafalsafa huko Ulaya vilikuwa vikijadili: Je, mwanamke ana roho kama roho ya mwanamume? Je, ana roho ya mwanadamu au mnyama? Na wakahitimisha mjadala wao kuwa mwanamke ana roho. Lakini roho hiyo ni duni sana kuliko roho ya mwanamume."



# NI UPI UJUMBE ULIOBAKIA?

Dini zote zimejiita kwa jina la mwanzilishi wake au kwa jina la taifa alilotumwa, hivyo basi kunasibishwa jina "Zoroaster" kwa dini ya uzorosti (Zoroastianism) na"Budha" kwa ajili ya dini ya Ubudha, na kwa sababu Uyahudi ulitokeza kwa kabila la Yahudha (Jehova), ndio maana ukaitwa Uyahudi na Ukristo kutokana na Kristo, tofauti na Uislamu ambao haujafungamanishwa na mtu au taifa fulani, bali kila mwenye kujisalimisha kwa Allah Mtukufu, na kutekeleza maamrisho yake na kukatazika na makatazo yake, mwenye kunyenyekea kwake peke yake, basi mtu huyo atakuwa amejisalimisha nafsi yake kwa Allah Ta'ala.

Yule ambaye atamfuata Mtume wa mwisho Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) na akaelekea katika dini ya haki ambayo amekuja nayo, na kuamini na kumfuata; huyo ndie Muislamu wa kweli, vyovyote awavyo katika zama zozote au mahala popote, na katika rangi yoyote au jinsia yoyote ile.

## Mwenyezi Mungu hana Mshirika.

"Hakuna Mungu isipokuwa Allah peke yake hana mshirika. Yeye haki na kila asiyekuwa yeye ni batili, ametuumba na ameturuzuku. Uislamu ni kujisalimisha kwa Mungu, kumnyenyekea yeye, kutulia kwake na kumtegemea yeye tu–na kuwa nguvu yote iko katika (istiqama) kunyooka katika hekima yake, na kuridhika kwa mgawo wake kadiri itakayokuwa katika dunia hii na katika akhera. Na kwa kadiri yoyote Allah atakavyotupa mtihani (na hata ikiwa ni mauti) basi inatakiwa kupokea hayo nyuso kunjufu na nafsi zenye ghera, zenye kuridhia vile vile na kujua kuwa hayo ni kheri na kuwa hakuna kheri zaidi ya hayo, kwani ni upumbavu mtu kuweka ndani ya akili yake dhaifu mizani ya Ulimwengu na hali zake, bali ni juu yake kuamini kuwa Ulimwengu una sheria adilifu, na hata kama itapotea katika ufahamu wake, na ya kuwa kheri ndio msingi wa ulimwengu, na kutengeneza (Islahi) ni roho ya ulimwengu…ni juu yake kufahamu hayo na kuamini na kufuata katika utulivu na Ucha-Mungu."

**Thomas Carlyle**
Mwandishi wa Mwanahistoria wa Scotland.



**Hakuna tofauti kati ya Muarabu na Muajemi.**

"Waislamu, hawaonani wageni vyovyote vile watakavyotofautiana mataifa yao, vivyo hivyo katika miji ya Waislamu (Daarul Islam) hakuna tofauti kati ya Mchina Muislamu na Muarabu Muislamu katika kufaidi haki zao. Kwa sababu haki za Kiislamu zinatofautiana na haki za wazungu (Ulaya) na hii ni tofauti ya msingi kabisa."

**Gustaf Lubon**
Mwanahistoria wa Kifaransa.



## UJUMBE ULIOBAKIA NDILO UMBILE LA ULIMWENGU

Uislamu ndio mwendo unaokwenda nao ulimwengu huu, Allah amesema: {Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumt'ii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?} [3:83],

Kwa hiyo inafahamika kuwa kila kitu hapa ulimwenguni kinafuata kanuni maalumu, na mwendo maalumu thabiti; hivyo basi jua, mwezi, nyota, ardhi na sayari nyingine zipo chini ya kanuni za kudumu (zisizobadilika) haziwezi kujiondosha au kutembea nje ya mzunguko wake walau kwa kadiri ya unywele, hata mwanadamu kama utazingatia hali yake itakubainikia wewe kuwa ananyenyekea utaratibu wa Allah unyenyekevu kamili.

Mwanadamu huyu hapumui wala hahisi haja yake ya maji, chakula, mwanga, joto ila kulingana na makadirio ya Allah yaliyopangilia maisha yake kwa utaratibu maalumu, na makadirio haya ndiyo yanayoongoza viungo vyake vyote; hivyo basi wadhifa na kazi mbali mbali zifanywazo na viungo hivi havisimami vyenyewe ila kulingana na alichokadiriwa yeye na Allah.

Makadirio hayo ya jumla yenye kukusanya ndio ambayo mwanadamu anajisalimisha kwake wala hakiondoki kitu katika utiifu wake katika



ulimwengu huu, kuanzia sayari kuwa mbinguni hadi punje ndogo ya mchanga ardhini, yote ni katika makadirio yake Mwenyezi Mungu Mfalme Mtukufu mwenye kukadiria mambo; ikiwa vitu vyote mbinguni na ardhini na yaliyo baina yake huongozwa na makadirio haya, inatubainikia kuwa; Uislamu ni dini ya Ulimwengu wote; kwa sababu Uislamu una maana ya kufuata amri ya mwenye kuamrisha na kuacha makatazo yake bila ya kupinga. {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [45:13].

Ama mwanadamu ambaye hamjui Mola wake na anakana uwepo wake pamoja na dalili zake, au kuabudu asiyekuwa Yeye na kumshirikisha na asiyekuwa Yeye, apende asipende mtu huyo anakuwa amejisalimisha kwake kwa maumbile yake aliyoumbiwa nayo.

Ama mwanadamu anashindana na mambo mawili:

Jambo la Kwanza:

Ni maumbile ambayo Allah amewaumbia nayo wanadamu kama vile kujisalimisha, kunyenyekea, na mapenzi ya kumuabudu Yeye Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na kujikurubisha kwake.

Kadhalika kupenda anavyopenda Allah kama vile haki, kheri, ukweli, kuchukia anachokichukia Allah ikiwemo batili, shari, jeuri, dhuluma na yanayofuata hayo katika nyenzo za maumbile ya mwanadamu kama kupenda mali, familia, watoto, hamu ya kula na kunywa, kuoa na yanayohitajiwa katika hayo ili viungo vya mwili kufanya kazi zake.



Jambo la Pili: Matakwa ya mwanadamu na Uchaguzi wake, wakati ambapo Allah amekwisha mtumia Mtume na kumteremsha vitabu; ili apambanue baina ya haki na batili, uongofu, upotevu, kheri na shari, na akampa akili na ufahamu ili awe na uoni katika uchaguzi wake; akipenda atafuata njia ya kheri ambayo itampeleka katika haki na uongofu, na akipenda kufuata njia ya shari ambayo itamwongoza katika shari na maangamizi: {Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae. Hakika Sisi tumewaandalia wenye kudhulumu Moto ambao utawazunguka kama khema. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyo tibuka. Yatayo wababua nyuso zao. Kinywaji hicho ni kiovu mno! Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno!} [18:29].

Kwa hiyo ukimuangalia mwanadamu kwa mazingatio ya jambo la kwanza utaona kuwa ameumbwa juu ya kujisalimisha, umbile lake linampelekea katika kufuata na kulazimika, wala hawezi kwenda kinyume nayo hali yake ni kama hali za viumbe wengine.

Ukimuangalia kwa kupitia muono wa pili utamuona ni mwenye hiari; anachagua anayoyataka, kwa hali hii ni kuwa ima awe ni Muislamu au awe ni Kafiri, Allah Ta'ala amesema: {Hakika Sisi tumembainishia Njia. Ama ni mwenye kushukuru, au mwenye kukufuru.} [76:3];

Kwa hiyo utakuta watu wanagawanyika sehemu mbili:

Mwanadamu mwenye kumjua Mola wake, anamuamini kuwa ni Mola wake, Mfalme wake na mola wake anayemuabudu Peke Yake, na anafuata sheria yake katika maisha yake ya uchaguzi, kama vile ambavyo yupo katika maumbile ya kujisalimisha kwa Mola wake, ambapo hawezi kwenda nayo kinyume, akifuata makadirio yake, na huyu ndie Muislamu aliyekamilika ambae ameukamilisha Uislamu wake, na hapo ndipo elimu yake ilipokuwa sahihi; kwani amemjua Mola na Muumba wake ambae amemtumia Mitume na kumpa uwezo elimu na kujifunza, na hivyo akili yake ikawa sahihi na

rai yake kuwa nzuri, kwa sababu ameitumia fikra yake, kisha akaamua kutomuabudu yeyote ila Allah ambae amemkirimu kipawa cha ufahamu na rai katika mambo, hivyo basi ulimi wake ukawa sahihi wenye kutamka haki kwa sababu hakiri isipokuwa uwepo wa Mola mmoja tu ambaye ni Allah Ta'ala ambaye amemneemesha uwezo wa kuzungumza na kutamka.

Ni kama kwamba maisha yake yaliyobakia hayakubaki isipokuwa ukweli tu kwani anafuata sheria ya Allah katika mambo ambayo mwenyewe ana hiari nayo, na ukaenea baina yake na viumbe wengine ulimwenguni mtangamano wa kufahamiana na kuliwazana pamoja.

Kwa sababu hamuabudu isipokuwa Allah mwingi wa hekima, mjuzi, ambaye wanamuabudu na kunyenyekea na kufuata makaridio yake viumbe wake wote, na Allah amewadhalilisha kwa ajili yako ewe mwanadamu, Allah Ta'ala amesema: {Na mwenye kuuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa anafanya wema, basi huyo hakika amekwisha kamata fundo lilio madhubuti. Na mwisho wa mambo yote ni kwa Mwenyezi Mungu.} [31:22].



### Kamwe Havipo pamoja

"Sikuwa na hiari katika kulinganisha kati ya msingi wa tawhidi ya Allah katika taswira ya Qur-aan pamoja na itikadi ya utatu kama Mkristo. Nikaona kuwa msingi huu wa pili upo duni sana kulinganisha na msingi wa Uislamu. Na kutokea hapo kwa dhati kubwa nikaanza kupoteza imani ya Ukristo kwa kuzingatia kuwa kumuamini kwangu Allah ndio mwanzo na muhimu zaidi katika dini yoyote: Kwa hiyo Ikiwa kumuamini kwangu Allah nimekosea katika ufahamu wa dini sahihi, maana yake ni kuwa kila kitu kinakuwa ni mchezo ambao hauna maana."

**Najimu Ramoni**

Mhubiri wa Ghana





# UJUMBE ULIOBAKIA NI DINI YA MANABII NA MITUME WOTE:

Uislamu ni dini ambayo Allah ameiteremsha kwa wanadamu wote, Allah amesema: {…Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu} [22:34],

Nayo ni dini ya manabii na Mitume wote, Allah amesema: {Semeni nyinyi: Tumemuamini Mwenyezi Mungu na yale tuliyo teremshiwa sisi, na yaliyo teremshwa kwa Ibrahim na Ismail na Is-hak na Yaakub na wajukuu zake, na waliyo pewa Musa na Isa, na pia waliyo pewa Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi; hatutafautishi baina ya yeyote katika hao, na sisi tumesilimu kwake.} [2:136]

Mitume wa Allah wameiamini, na kutangaza Uislamu wao kwa Allah, na kuulingania, Allah amesema kuhusu Nuhu: {Wasomee khabari za Nuhu alipo waambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi na kukumbusha kwangu kwa Ishara za Mwenyezi Mungu kunakutieni mashaka basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Nanyi tengezeni mambo yenu pamoja na washirika wenu, na wala mambo yenu yasifichikane kwenu. Kisha nihukumuni, wala msinipe muhula. Lakini mkigeuka, basi mimi sikukuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waislamu.} [10:71-72],

Na kuhusu Ibrahim ('Alayhi Salaam) amesema: {Na Mola wake Mlezi alipo mwambia: Silimu, Nyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote.} [2:131],

Bali Ibrahim aliwausia hayo wanawe baada yake, Allah amesema kuhusu hilo: {Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu. Je! Mlikuwapo yalipo mfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is- hak, Mungu Mmoja tu, na sisi tunasilimu kwake. } [2:132-133]



Na kuhusu Musa ('Alayhi Salaam) Allah amesema: {Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.} [10:84]

Na amesema katika habari za Masihi ('Alayhi salaam): {Na nilipo wafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.} [5:111].

Uislamu ni ujumbe wa mwisho kutoka mbinguni kwa ajili ya wanadamu ambao amemtuma nao Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa watu wote, ambao Allah ameukamilisha na kuuridhia kwa waja kuwa ndio dini yao. Allah Ta'ala amesema: {…Leo nimekukamiliishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni UISLAMU uwe ndiyo Dini….} [5:3].



Katika aya hii tukufu Allah anaelezea kuwa amewaridhia wanadamu Uislamu kuwa ndio dini yao, na Allah akatangaza kuwa ndio dini ya haki, na ya kuwa hatokubali kwa yeyote dini isiyokuwa hiyo, Allah amesema: {Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu….} [3:19],

Na akasema vile vile: {Na anaye tafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri.} [3:85].

Katika aya ya kwanza anasisitiza kuwa dini anayoitambua ni Uislamu tu, na katika aya ya pili kuwa Allah hatokubali kwa yeyote dini isiyokuwa Uislamu, na kuwa watakaofaulu wakiwa na furaha baada ya mauti ni Waislamu peke yao, na ambao watakufa bila ya Uislamu watakuwa wamepata hasara katika akhera, na wataadhibiwa motoni; na kwa hili Mitume wote walitangaza Uislamu wao kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) na wakatangaza kuwa mbali na wale ambao hawakusilimu, atakayetaka kuongoka miongoni mwa Mayahudi na Manasara na kupata furaha basi asilimu na aingie katika Uislamu amfuate Mtume wa Uislamu Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ndipo awe mfuasi wa kweli wa Musa, Issa ('Alayhima salaam); kwani Musa, Issa, Muhammad na Mitume wote ni Waislamu, wote walilingania Uislamu, kwani ndio dini ya Allah aliowatuma kuifikisha kwa wanadamu, hivyo haifai kwa yeyote aliyepatikana na kuzaliwa baada ya Muhammad hadi mwisho wa dunia kuwa yeye amejisalimisha kwa Allah, wala Allah hatokubali madai hayo ila tu baada ya kumuamini Muhammad kuwa ni Mtume kutoka kwa Allah, na amfuate, na atende kulingana na Qur-aan ambayo Allah ameiteremsha kwake, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Naapa kwa ambae nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake, atayenisikia yoyote katika Ummah huu, awe Myahudi au Mnasara, kisha akafa na hakuniamini nilichoshushwa nacho, isipokuwa atakuwa katika watu wa motoni.» (Muslim).

## Uislamu ni Mwepesi.

"Hakika wepesi mkubwa wa Uislamu unatokana na tawhidi halisi. Katika wepesi huu ndio kuna siri ya nguvu ya Uislamu. Uislamu na ufahamu wake ni mwepesi umeepukana na yale tunayo yaona katika dini nyingine na akili iliyosalimika inakataa migongano na utata. Hakuna kitu kilicho wazi zaidi kuliko misingi ya Uislamu inayoeleza uwepo wa Mungu mmoja na usawa wa wanadamu wote mbele ya Allah."

**Gustaf Lubon**

Mwanahistoria wa Ufaransa.







# UKAMILIFU WA UJUMBE ULIOBAKIA:

Uislamu huu ambao Allah amemtuma nao Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa watu wote ni Dini ya kumuamini Allah na kumpwekesha, Allah Ta'ala amesema: {Yeye ndiye aliye Hai - hapana mungu isipo kuwa Yeye. Basi muabuduni Yeye mkimsafishia Dini Yeye. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote. Sema: Mimi nimekatazwa kuwaabudu hao mnao waomba badala ya Mwenyezi Mungu, zilipo nijia hoja zilizo dhaahiri kutokana na Mola wangu Mlezi. Na nimeamrishwa nisilimu kwa Mola wa walimwengu wote.} [40:65-66].

Ni dini ambayo waja humsafishia ibada Yeye Peke yake, Allah Mtukufu amesema: {Je, mabwana wengi wanao farikiana wao kwa wao ni bora au Mwenyezi Mungu Mmoja Mwenye nguvu? Hamuabudu badala yake ila majina tu mliyo yapanga nyinyi na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuyateremshia hayo uthibitisho wowote. Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu. Yeye ameamrisha msimuabudu yeyote isipo kuwa Yeye tu.} [12:39-40],

Nayo ni dini ya akili zilizosalimika lau ingedhihirishwa ukweli na usafi wake nafsi zingefuata kwa kutii na kujisalimisha, Allah Mtukufu amesema: {…Hiyo ndiyo Dini Iliyo Nyooka. Lakini watu wengi hawajui.} [12:40],

Ni dini ya dalili, hoja na uthibitisho: {…Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:64],

Ni dini ya raha na furaha na utulivu: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema…} [16:97].

Ndani ya dini ya Uislamu ambayo Allah amemtuma nayo Mtume Muhammad, Allah amehalalisha vizuri vyenye manufaa, na akaharamisha machafu yenye kudhuru, na akaamrisha kila mema na akakataza kila maovu na munkari. Uislamu ni dini nyepesi, hakuna mashaka ndani yake, wala taklifu, wala mzigo ambao watu hawawezi kuubeba, Allah Mtukufu amesema:

{Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii, asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa.} [7:157].

Ni dini kamilifu, iliokusanya yenye kufaa kwa zama na mahali pote hadi pale Allah atakapoirithi ardhi na vilivyomo. Imekuja na mahitaji yote ayahitajiayo mwanadamu katika dini na dunia yao.

Uislamu ni njia ya furaha na utulivu, njia ya elimu na ustaarabu, njia ya uadilifu na wema, ni njia ya karama na uhuru, njia ya kheri zote na wema.

Ni utukufu wa dini hii na ukamilifu wake!! Na ni dini ipi ni bora kuliko ile ambayo mja amejisalimisha kwa Allah Mtukufu? Allah amesema: {Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema, na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu?...} [4:125].



**Hakuna kumuabudu asiyekuwa Allah.**

"Navutika sana na Imani ya Uislamu ya Mungu mmoja. Hakuna kama Yeye. Imani hii ya Mungu Mmoja pekee inamuepusha mtu na kuwa mtumwa wa binadamu yeyote na huu ndio uhuru wa kweli. Ule uhusiano wa moja kwa moja kati ya Mungu na watumwa wake (waumini) ulinivutia vile vile."

**Ibrahim Khalil (Philobus)**
Padri na Muhubiri wa Misri.



**Dini na Dunia Viko Pamoja**

"Umoja huu wa kipekee ambao hauna mfano wake kwa taathira ya kidini na ya kidunia kwa pamoja, inamfanya Muhammad aonekane kuwa ni mtu mwenye haiba kubwa ya pekee yenye taathira katika historia ya wanadamu."

**Michael Hart**
Mwandishi wa Kimarekani



**Kwanini Isiwe Hivyo.**

"Ikiwa huu ndio Uislamu. Kwa nini basi sote tusiwe Waislamu."

**Goethe**
Mwanafasihi wa Kijerumani

Huu wito kutoka kwa Mola wako ambaye yeye ni Mwenye kukuhurumia wewe zaidi kuliko hata nafsi yako uliyo nayo. Anakulingania, kutoka kwenye kiza kwenda kwenye Mwanga, Allah Mtukufu amesema:

{Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.} [3:64].

Katika mkabala wa hilo mja ambae amejisalimisha kwa Allah kuna mtu Mwingine amekataa na kufunika umbile lake la Uislamu ambalo Allah amemuumba nalo kwa pazia la kupinga na kukanusha pamoja na mfululizo

wa dalili na miujiza inayoonesha usahihi wa dini hii.

Hivyo mtu huyu akajichagulia nafsi yake ushirikina kinyume na Tawhidi, kiza cha dhana, uzushi badala ya mwanga wa haki, yakini na uongofu, na kuridhia nafasi yake kuwa ni mtumwa wa waja mfano wake, kama vile watawa na wanazuoni wa kiyahudi, bali na Mitume badala ya kuwa ni waja wa Allah mmoja Peke yake; na hivyo basi fitra yake ikapotea na akili kupotea na kunyenyekea katika matamanio na utata huku akiacha fitra ya Allah ambayo Allah amemuumba nayo, hakuzaliwa mtoto yoyote ila katika fitra ya Uislamu:

{Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30].

Sasa ni juu yako kukadiria ndani ya nafsi yako kilichomtumbukiza kafiri kwenye upotevu wa wazi: {Yeye ndiye aliye kufanyeni manaibu katika ardhi. Na anaye kufuru, basi kufuru yake ni juu yake; na kufuru za makafiri haziwazidishii kwa Mola wao Mlezi ila kuchukiwa. Wala kufuru za makafiri haziwazidishii ila khasara.} [36:39]

**Imani ya Muhammad juu ya Ujumbe Wake.**



"Huenda wale wafalme na watawala ambao walipokea barua waliingiwa na mshangao kutokana na mtu huyu asiye na makuu ambae aliwaita kwenye utii. Kutuma barua hizi kunatupa picha ya kiasi cha kujiamini kwa Muhammad mwenyewe na ujumbe wake. Aliuandalia Umma wake kwa kujiamini huku na imani hii ni nguvu, utukufu na ulinzi, pembezoni mwake ni wakazi wa majangwani kubadilika kuwa mabwana waliofungua nusu ya Ulimwengu uliokuwa ukijulikana katika zama zao. Muhammad alifariki baada ya kuyafanya makabila yote ya Kiarabu yaliyotawanyika kuwa Ummah mmoja wenye ghera na hamasa."

**Jawaharlal Nehru**

Waziri Mkuu wa Kwanza India.



## Ni ipi misingi na rejea na sifa za Ujumbe huu?

# MISINGI YA UWEKAJI SHERIA



Uwekaji sheria wa Kiislamu umesimama katika misingi na nguzo za aina yake ambazo zinamfaa mwanadamu yeyote wa zama na mahala pote, na misingi ile muhimu ni hii ifuatayo:

## Kwanza: Kurahisisha (Kufanya wepesi) na kuondosha Uzito.

Majukumu yote ya kisheria hayatoki nje ya uwezo wa wale waliokalifishwa na nafasi yao, wala haimbebeshi mtu mzigo au kumtoa katika mazoea katika kazi za kawaida, kwani dini ni nyepesi, Allah Mtukufu amesema:

{…Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito…} [2:185],

Na Allah tena akasema: {Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.} [4:28],

Na tena Allah Mtukufu akasema: {Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yoyote ila kwa kadiri ya iwezavyo…} [2:286].Mama Aisha



**Ujumbe wa Utume wa Muhammad.**

"Muhammad alitumia muda wake wote kufanikisha ujumbe wake katika kudhamini hizi mandhari mbili katika mazingira ya jamii yake ya kiarabu, hayo mawili ni Umoja katika Fikra ya dini, kanuni na nidhamu ya utawala na hukumu. Yote yalitimia kwa fadhila za nidhamu ya Uislamu ambayo ulibeba mgongoni mwake umoja na utawala wenye mamlaka kwa pamoja. Uislamu ukawa na nguvu kwa fadhila hiyo, nguvu yenye msukumo na utisho imewahamisha waarabu kutoka kwenye umma wa kijahili na kuwa ulioendelea."

**Arnold J. Toynbee**

Mwanahistoria wa Uingereza

(Radhiya LLahu 'anha) amesema: «Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hakukhiyarishwa kati ya mambo mawili ila alichagua jepesi zaidi, madamu si dhambi, ikiwa ni dhambi alikuwa mbali nayo sana, Wallahi hakulipa kisasi kwa ajili ya Nafsi yake jambo aliloletewa katu, hadi pale ambapo Sheria ya Allah itakapovukwa, hivyo kulipa kisasi kwa ajili ya Allah» (Al-Bukhari).

Miongoni mwa kuondoa uzito (Mashaka) katika sharia ya Kiislamu ni majukumu machache; kiasi cha kumuwezesha mwenye kukalifishwa kusimamia majukumu yake bila ya uchovu au taabu; kwani katika uchovu kuna mashaka na dhiki, na mashaka huondoshwa, Allah Mtukuka amesema: {…Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini…} [22:78],

Kama ambavyo malengo ya majukumu ya kisharia ni kumpelekea mwenye kutekeleza majukumu yake katika maisha ya furaha duniani na akhera, hivyo basi sharia haileti jukumu ila kulingana na kinachowezekana kwa maumbile na tabia ya mwanadamu, Allah Mtukuka amesema:



**Akida iliyokita.**

"Katika nguzo tano za Uislamu hakuna kitu kinachochukiwa na asiyekuwa Muislamu. Pamoja na wepesi wa faradhi hizi na uchache wa idadi yake, hakukuwa na haja ya kuingiza marekebisho yatakayoiongoza kwenye kuithibitisha imani ya Kiislamu katika nafsi ya kila Muislamu. Hakika ubobezi wa kielimu kwa imani ya Kiislamu ina dalili ya dhati kutokana na nguvu yake, kubakia na kuenea kwake."

**George Sarton**

Muhadhiri wa Vyuo Vikuu vya Washington na Harvard.





**Dini Kwanza.**

“Misingi ya tabia ya Kiislamu, sheria na serikali yao. Vyote vimesimama juu ya misingi ya dini: Uislamu ni dini nyepesi zaidi na ya wazi kuliko dini nyingine. Na msingi wake ni kushuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na Muhamad ni Mtume wa Allah.”

**Will Durant**

Mwandishi wa Kimarekani



{Enyi mlio amini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na mkiyauliza inapo teremshwa Qur’ani mtabainishiwa. Mwenyezi Mungu amesamehe hayo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghfira Mpole. Waliyauliza hayo watu wa kabla yenu, kisha wakawa wenye kuyakataa.} [5:101-102].

## PILI: KUCHUNGA MASLAHI YA WATU:

Mwenye kufuatilia hukumu za sheria ya Kiislamu itamdhihirikia kuwa muradi wake ni kufanikisha maslahi ya watu; kiasi cha kuwafanikishia watu kheri na wema, na hivyo basi kuondosha shari, ufisadi duniani na akhera, kwa mtu binafsi na kwa jamii yote katika zama na mahali pote, Allah Mtukuka amesema: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Kwa hiyo rehema ni kwa ajili ya kufanikisha maslahi, vinginevyo kama rehema isingekuwa ndio makusudio yake, basi Mtume (Swala Llahu ‘alayhi wasallam) asingesifika kuwa Nabii mwenye rehema, na majukumu yote yanarejea katika maslahi ya waja duniani na katika akhera yao; kwa sababu Allah anajitosha kwa

waja wake wote, hivyo basi utii haumnufaishi wala maasi hayamdhuru.

Sharia yote ni adilifu, ina kila aina ya huruma, maslahi na hekima; na suala lolote lililotoka kwenye uadilifu kwenda kwenye dhuluma, kutoka kwenye dhuluma na rehema kwenda kinyume chake, na kutoka kwenye maslahi kwenda kwenye uharibifu na ufisadi, na kutoka kwenye hekima kwenda kwenye upuuzi hayo si katika sharia.

## TATU: KUTIMIZA UADILIFU KWA NJIA ZOTE:

Maandiko mengi yameshirikiana kuthibitisha nafasi ya Uadilifu kama mfumo wa jumla kwani tunapata maandiko yenye kulingania kusimamisha uadilifu, na mengine yenye kukataza dhuluma, hata ikiwa ni pamoja na mtu mwenye kuhalifu, Allah Mtukuka amesema: {Enyi mlio amini! Kuweni wasimamizi madhubuti kwa ajili ya Mwenyezi Mungu mkitoa ushahidi kwa haki. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamngu. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za mnayo yatenda.} [5:8].

## NNE: KUENEA NA KUKAMILIKA.

Kwa hakika miongoni mwa yanayoonesha kusihi dini hii ni kule kujipambanua kwa upana na ukamilifu wake, Allah Mtukuka amesema: {…Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote…} [6:38],

Na akasema vile vile: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89],

Na kuenea huku kunaonekana katika akida na taswira, na katika ibada na kujikurubisha, na katika Akhlaki na fadhila, (ubora katika maeneo yote) na katika uwekaji sheria, oganaizesheni na hukumu mbali mbali, si hivyo, bali katika maisha yote.

## TANO: USAWA NA ULINGANIFU:

Dini ya Uislamu ni dini ya usawa na ulinganifu: {Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani…} [2:143],

Na kila kitu katika hukumu zake zimetayarishwa katika mizani makini: {Na mbingu ameziinua, na ameweka mizani} [55:7]

Na Allah amewaamrisha Waislamu kusawazisha kila kitu, miongoni mwa hayo kauli yake Allah Mtukuka: {Na wale ambao wanapo tumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo} [25:67],

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amekataza Ghuluu (kupetuka mipaka): Akasema:

"Tahadharini kuzidisha katika dini kwani (ghulu) kuzidisha imewaangamiza waliokuwa kabla yenu."

Na akaamrisha usawa na kumpa kila mwenye haki, haki yake. Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): "Hakika Mola wako ana haki juu yako, na Nafsi yako ina haki juu yako, na kwa familia yako ina haki juu yako, hivyo mpe kila mwenye haki haki yake."



**Uislamu… Ni amani na salama.**

"Mayahudi chini ya bendera ya Uislamu walipata amani na uadilifu ambayo iliwazuia na shari ya uadui na kukandamizwa, na Karne nyingi zilipita wakiwa katika kheri nyingi."

**Naseem Souza**

Mhadhiri wa Kiiraqi, Myahudi



# SIFA ZA UWEKAJI SHARIA WA KIISLAMU:

## KWANZA: INATOKA KWA MUNGU:

Chanzo cha dini ya Kiislamu ni Muumba Mtukufu Aliyemuumba mwanadamu na Ulimwengu na vilivyomo ndani yake, na kuwa kwake imetoka kwa Mwenyezi Mungu ina ipa hadhi nyingi, miongoni mwake ni kuwa Allah ndie Muumba na ndie mtoa riziki, yeye pekee ndiye mwenye kumiliki haki ya uwekaji sheria.

Mitume wote na wafuasi wao wakitegemea mwekaji sheria kutoka kwa Allah pekee, na hubatilisha kila sheria isiyotoka kwake, Allah akimuelezea Mtume wake wa mwisho kuhusu sheria yake na muelekeo wake: {Sema: Mimi si kiroja miongoni mwa Mitume. Wala sijui nitakavyo fanywa wala nyinyi. Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi.} [46:9]

Kwa hiyo Mtume wa Allah pamoja na utukufu wa hadhi yake na nafasi yake ya juu kwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anafuata sheria ya Allah anayoshushiwa yeye wahyi, yeye sie mwanzilishi, bali hufuata mfumo wake na wala haendi kinyume nao, na kuwa Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ndie Muumba anajua aliowaumba: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14]

Yeye anajua maumbile ya waja wake na yanayowafaa na yanayowaharibu, anajua zaidi yanayowanufaisha na yanayowadhuru, hakuna mwingine anayewafahamu zaidi ya aliyewaumba, na hakuna zaidi ya mtengezaji anajua zaidi yake alichokitengeneza. Allah Mtukufu amesema: {…Sema: Je, nyinyi mnajua zaidi au Mwenyezi Mungu?...} [2:140].

Na kwa sababu Allah ndie aliyeweka sheria, hii inaipa sheria yenyewe uadilifu na ukweli wake. Kamwe haiwezekani Allah ampendelee mja miongoni mwa waja wake kwa ajili ya hesabu ya mja mwingine, kama ambavyo adhabu ilivyo katika Uislamu basi Yule ambaye hakuchukua haki yake duniani kwa sababu yoyote au ambaye hajaadhibiwa duniani kwa ubaya wa matendo yake, basi atakuta malipo yake akhera.

## PILI: UHUSIANO WA UWEKAJI SHERIA NA MAADILI:

Lengo la kanuni yoyote ni kuwa kanuni haifikiwi malengo yake kwa maumbile yake bali hutegemea mwitikio wa watu wa kutekeleza kanuni na sharia ile kwa ridhaa yao na kukinai kwao, kama vile ambapo lengo la kanuni husika halifikiwi kwa uzuri wa hukumu zake pekee, lakini hufikiwa pamoja nayo kwa utekelezaji wa wale waliowekewa sheria ile, kwa sharti ya kuwa utekelezaji huu uwe unatoka ndani ya Nafsi zao na mioyo yao.

Hisia hii hutokana na imani yao ya kuwa kanuni yenyewe ni ya uadilifu na kuiridhia kwao, na itikadi ya kulipwa na mtunga sheria nao wakiridhia sheria zake na hukumu zake mbali mbali. Sheria ya Kiislamu imesimama katika kuridhiwa na kukinai kwa watu wenyewe, Allah ameamrisha kufundishwa Uislamu: {…na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.} (4:63), {Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia.} [87:21 – 22],



**Dini ya Utulivu.**

"Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu nimehisi amani na utulivu na kuwa ndani ya maisha yangu kuna thamani. Nimefahamu maana ya kuwa Mungu (Allah) ambae humuoni yeye anakuona popote uwapo na huangalia matendo yako na huyapima kwa vipimo vya uadilifu ili upate malipo yako ya haki Siku ya Kiama."

**Anatoli Andrbush**
Jenerali wa Kirusi

ndio maana Allah akaufunga Ujumbe wa Muhammad na kutumwa kwake kwa sababu hii; Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasalaam): "Kwa hakika nimetumwa kutimiza tabia njema."

## TATU: UHUSIANO WA DUNIA NA AKHERA:

Miongoni mwa sifa zinazopambanua sharia ya Kiislamu dhidi ya sheria ziliotungwa na wanadamu ni kuwa (Sharia ya Kiislamu) humlipa mwanadamu katika maisha ya hapa duniani na katika akhera vile vile, malipo ya akhera ni makubwa kuliko ya dunia; kwa ajili hiyo daima muumini anahisi hili na



kumsukuma ndani ya Nafsi yake katika ulazima wa kutekeleza hukumu zake, kufuata maamrisho na makatazo yake na kama atakwepa malipo katika maisha ya duniani hujua fika kuwa macho ya Allah hayaghafiliki wala kulala, na kuwa watu watachukuliwa kwa wayatendayo hapa duniani mbele ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) Allah Aliyetukuka amesema: {Ati anadhani hapana yeyote ataye muweza?} [90:5]

Na akasema vile vile: {Ati anadhani ya kuwa hapana yeyote anaye mwona?} [90:7]

## NNE: SIFA YA KIJAMII KATIKA HUKUMU ZAKE:

Sheria ya Kiislamu haipendelei maslahi ya sehemu moja zaidi ya sehemu nyingine wala haimpendelei mtu mmoja dhidi ya mwingine, imeweza kutatua tatizo hilo kubwa ambalo jamii zingine mbali mbali linasumbuka nalo.

Tatizo la mgongano kati ya maslahi ya mtu binafsi na maslahi ya Ummah katika jamii kama tuonavyo katika mfumo wa Kibepari wakati ambapo katika mfumo wa Kijamaa kupendelea masilahi ya jamii na kupuuza masilahi ya mtu binafsi na kupoteza na kuvunja haki ya mtu binafsi na hivyo kutupa haki ya mtu binafsi na uhuru wake na haki ya kumiliki, na hivyo basi vipaji vyake kutojitokeza na kupotea kwa utu wake na kupelekea kutotumika kwa uwezo wa mtu binafsi.

Lakini Uislamu umeweka haki kwa msingi wa usawa baina ya haki hizi za kijamii (haki) ambayo inaisimamisha; Uislamu umechunga maslahi ya jumla ya jamii ya Kiislamu, hata hivyo wakati huo huo haujaghafilika



na matakwa ya Muislamu binafsi.

Katika upande wa kisiasa tunaona kuwa haki ya mtawala na kiongozi ni kupata kusikilizwa na raia zake na kutiiwa, lakini kwa sharti la kufuata sheria katika kuhukumu kwake huku akichunga maslahi ya Ummah.

Vinginevyo Uislamu unamnyang'anya haki hii; hivyo basi itapasa kumtii mtawala au kiongozi katika yasiyokuwa kumuasi Allah (Subhaanahu wa Ta'ala).

## TANO: UTHIBITI KATIKA KANUNI NA ULAINI KATIKA UTEKELEZAJI:

Uislamu umesimama juu ya misingi thabiti isiyobadilika inachukuwa vyanzo vyake kutoka katika misingi yake ya mwanzo:

Qur-aan iliyohifadhiwa na Allah: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9],

Ambayo haingiliwi na batili yoyote: {Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake. Kimeteremshwa na Mwenye hikima, Msifiwa. } [41:42].

Sunnah tukufu imerikodiwa nakuhifadhiwa kwa undani na umakini mkubwa na maandiko yake (nususi) mara nyingi hukusanya hukumu za uwekaji sheria bila ya kubainisha vipengele vinavyohusiana na utekelezaji wa



hukumu hizo; na hivyo kuacha uwezo mkubwa wa utawala na kukadiria kwa Mujtahidi akichunga tofauti za hali na mazingira, hata hivyo utekelezaji wa hukumu hizi bado umebaki katika kuangalia wasaa na kutokakamaa katika jambo.

Kwani lililo la msingi ni kutekeleza malengo haya bila ya kujali njia zitakazotumia au maumbo yaliyosimamia madamu hayaendi kinyume na andiko la kisheria au msingi miongoni mwa misingi ya kisheria ya Kiislamu, kwa hiyo utekelezaji wa makusudio ya jumla ya sheria ya Kiislamu kwa daraja ya juu ya wepesi na uwezekano wa kuendelea (kukua) kadhalika hakuna kizuizi katika kutokea kwa hukumu mpya ambayo haikujulikana hapo kabla kwa kuangalia kuzuka mazingira yanayoafikiana nayo.



## Dini ya Utukufu na Ukarimu

"Uislamu ni dini ya amani, usawa, uhuru, udugu, ukarimu na utukufu, yote hayo yanaonekana wazi kwenye hukumu zake, misingi yake na taratibu zake, kwa mfano Saumu katika Uislamu si kama saumu katika dini nyingine, kwa sababu matatizo ya mwanadamu si (mtu) kukandamiza mahitaji ya mwili wake kama vile wafanyavyo watawa kiasi kwamba kiwiliwili cha mmoja wao kinakuwa kama vile hekalu la mifupa inayotembea. Uislamu umenyoosha matamanio ya kiwiliwili na haujayakandamiza; Saumu katika Uislamu unazoesha nafsi ya mfungaji kusubiri na Jihadi dhidi ya matamanio maovu yaliyoharamishwa, na kumchunga Allah katika siri na dhahiri na kujitambuza ladha ya kukosa na njaa, ili mfungaji awaonee huruma waliokosa, kama ambavyo Saumu ni fursa ya kuupa mwili raha dhidi ya kuvimbiwa. Saumu humfaidisha mtu afya yake, roho yake na akili, na katika yote kuna kujiburudisha kwake, na umoja wake."

**Berisha Pennekmrt**

Mwanataaluma wa Kithailand aliyetoka kwenye Ubudha na kuingia Uislamu.



# SHERIA YA KIISLAMU NA KANUNI ZA WANADAMU… TOFAUTI ZILIZOPO:

Kuna tofauti na kuhitilafiana Sharia ya Kiislamu na sheria zilizowekwa na wanadamu.

### 1. Haiba, Utukufu na kuheshimu Nafsi za watu:

Sharia ya Kiislamu inasifika kwa kuwa na haiba na utukufu wa kujali utu wa mwanadamu, na hivyo inatokana na sifa ya kidini iliyoshikamana nayo na kwa sababu muwekaji wake ni Allah ambaye yeye nafsi za wanadamu zinanyenyekea kwake na kutukuzwa.

### 2. Sharia kukubaliana na maumbile (fitra) kwa zama zote na mahala pote:

Sharia ya Kiislamu ni kwa ajili ya Ummah na mataifa yote kwa tofauti zao zilivyo, tabia, mazingira na lugha-wanayozungumza; kwa sababu muwekaji wake (sharia hii) ni Allah (Subhaanahu Wa Ta'ala), naye ni mjuzi wa yaliyopo na yajayo kwa maumbile yao na silika ya tabia zao na kila chenye kuhusiana nao pamoja na kutakasika kwake kutawaliwa na matamanio, Allah amesema: {Basi uelekeze uso wako sawasawa kwenye Dini - ndilo umbile la Mwenyezi Mungu alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo Dini iliyo nyooka sawa. Lakini watu wengi hawajui.} [30:30],

Ama sharia hizi za wanadamu zimewekwa na mwanadamu nao pamoja na elimu kubwa waliyofikia elimu yao hiyo ina upungufu na hata wakijua ya jana yao na mambo yao ya leo, hawawezi kujua ya kesho yalivyo, na hata wakijua tabia za baadhi ya watu hawawezi kujua yote, katika hali hii. Sheria za wanadamu hazilingani na maumbile yote ya mwanadamu wala hazilingani na mazingira yote, na ikiwa sheria hiyo imefaa kutumika kwa watu fulani haifai kutumika kwa wengine….

### 3. Sharia ya Kiislamu kuafikiana na haki na uadilifu.

Sharia ya Kiislamu inaafikiana na usawa, haki na uadilifu na hiyo ni kutokana na kutowezekana kutokea makosa, au dhuluma au kutawaliwa na matamanio na hamasa za watu, Allah Mtukuka amesema: {Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu. Hapana awezaye kuyabadilisha maneno yake. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia na Mwenye kujua.} [6:115],

Allah pekee ametakasika kuepukana na malengo (matamanio), mwenye kujua mambo yaliyofichikana na yaliyodhihiri, yeye ndie amezunguka mambo ya waja, hawezi kuamrisha ila lenye maslahi yao, wala hakatazi ila lenye kuwadhuru. Ama kanuni na sheria waliyojitungia wanadamu hukumbwa na makosa, usahaulifu, na kufuata matamanio ya watu, hivyo ni vigumu kusalimika na makosa, upungufu na mabadiliko, Allah Mtukuka amesema: {… Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangeli kuta ndani yake khitilafu nyingi.} [4:82].

### 4. Sharia kujali utu wa mwanadamu:

Sharia ya Kiislamu sio kanuni tu zilizowekwa na fikra za watu, lakini muwekaji wake ni Allah Aliyetukuka katika yale yaliyo mnasaba na mwanadamu na tabia yake na maumbile yake, Aliyeumba watu anafahamu zaidi yenye kunasibiana nao, {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14],

Naye anajua zaidi anachomrahisishia: {Mwenyezi Mungu anataka kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.} [4:28].

Ama sheria za wanadamu zimewekwa kulingana na matakwa ya aliyeiweka, na kulingana na umuhimu na mazingira yake.

### 5. Uhusiano wa Sharia ya Kiislamu na upande wa kiroho:

Sharia ya Kiislamu inahusiana na matendo ya dhahiri na matendo ya ndani ya mwanadamu; Allah Mtukuka amesema: {…Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zenu. Basi tahadharini naye….} [2:235].

Kinyume na sheria za mwanadamu ambazo zinajihusisha na matendo ya nje ya mwanadamu tu na hayajali upande wa kiroho hata kidogo, ama adhabu zinazotolewa na sharia hizi za mwanadamu ni za kidunia tu.



## Jamii (Safi) yenye furaha.

"Jamii ya Kiislamu ambayo inajilazimisha kufuata hukumu na adabu zake, ni jamii nadhifu yenye furaha, ni jamii ambayo ndani yake hakuna jinai kwa rangi zake zote."

**Berisha Pennekmrt**

Mwanataaluma wa Kithailand aliyebadilisha Ubudha na kuwa Muislamu.



# VYANZO VYA UISLAMU.

Dini ya Kiislamu inapokea sheria yake, akida zake na hukumu katika ufunuo (Wahyi), kutoka kwa Mwenyezi Mungu (Qur-aan na Sunnah) hizo ndizo vyanzo vikuu viwili vya msingi vya Uislamu, na kutoka katika vyanzo hivyo ndio imepatikana sheria yake, itikadi zake na hukumu zake, ifuatayo ni taarifa zake kwa ufupi.

## A. QUR-AAN TUKUFU:

Allah ameteremsha Qur-aan kwa Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) kuwa muongozo kwa wamchao Mungu, desturi ya Waislamu, tiba ya nyoyo ambayo Allah ametaka kuwapa uongofu na taa kwa yule ambaye Allah amemtakia kufanikiwa na mwangaza.

Nayo inakusanya misingi ambayo kwa ajili yake Allah ametuma Mitume, na Qur-aan sio kitabu kilichozushwa miongoni mwa vitabu kama ambavyo hakuwa Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasalaam) Mtume miongoni mwa Mitume aliyezuka tu; Allah alishateremsha kwa Ibrahim Suhufi (maandiko), na akamkirimu Musa Taurati na Dawuud Zaburi na Issa akaja na Injili.

Vitabu hivi ni Ufunuo (Wahyi) kutoka

**Qur-aan ....Kitabu cha Mwisho cha Mbinguni.**

"Nilipoamini tawhidi nikaanza kutafuta hoja na dalili mbali mbali ambazo zinathibitisha kuwa Qur-aan ni kitabu cha Mwenyezi Mungu Aliyetukuka na kuwa Qur-aan ni kitabu cha Mwisho. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutatua mas-ala haya: Qur-aan Tukufu ni kitabu pekee ambacho kinakubali na kutambua vitabu vyote kutoka mbinguni, wakati ambapo vitabu vyote vinapinga vitabu vingine. Kwa hakika hii ndio moja ya sifa kubwa inayopambanuka Qur-aan Tukufu."



**Bashir Shaad**
Muhubiri wa India.



## Nafasi ya Qur-aan na fadhila zake.

"Qur-aan imebakia karne kumi na nne imehifadhiwa katika kumbukumbu ya Waislamu ikihamasisha fikra zao, kutengeneza tabia zao, na kuchochea hamasa za mamia ya milioni ya watu, Qur-aan inaweka katika nafsi za watu imani nyepesi zaidi yenye utata mchache ambao ipo mbali na vifungo vya rasimu na mafundisho ya Kikristo.

Qur-aan imekuwa bora katika kunyanyua viwango vya tabia za Waislamu na elimu. Na ndio iliyosimamisha ndani yao kanuni za mfumo wa kijamii na umoja wake, na kuwahimiza kufuata kanuni za afya na kufungua akili zao kutokana na dhana potofu na dhuluma na ususuavu (wa nyoyo) na kutengeneza vizuri hali za watumwa na kuingiza katika nafsi za wanyonge heshima na utukufu."

**Will Durant**
Mwandishi wa Kimarekani

kwa Allah amewafunulia Mitume wake, na kinachothibitisha kuwa Qur-aan hii ni Wahyi kutoka kwa Allah, ni kuwa inathibitisha imani ya kila Mtume wa Allah wala haitofautishi kati yao, Allah amesema: {Hakika wale wanao mkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya, Hao ndio makafiri kweli. Na tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha. Na walio muamini Mwenyezi Mungu na Mitume wake, wala wasimfarikishe yeyote kati yao, hao atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira, na Mwenye kurehemu. } [4:150-152],

Isipokuwa vitabu hivi vilivyotangulia vingi vimepotea na kuharibika sehemu yake kubwa na vikaingiliwa na kubadilishwa na kugeuzwa.

Ama Qur-aan Tukufu Allah amedhamini hifadhi yake Allah Mtukufu amesema: {Hakika Sisi ndio tulio teremsha Ukumbusho huu, na hakika Sisi ndio tutao ulinda.} [15:9],

Na akaifanya iwe ufunuo na kufuta vitabu vilivyotangulia katika vitabu, Allah amesema: {Na tumekuteremshia wewe, kwa haki, Kitabu hichi kinacho sadikisha yaliyo kuwa kabla yake katika Vitabu na kuyalinda…} [5:48],

Na yule aliyeiteremsha akaisifu kuwa ni ubainisho wa kila kitu; kwa hiyo Allah akasema: {…Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu.} [16:89].

Ni muongozo na rehema; Amesema Allah: {…Basi imekufikieni bayana kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na uwongofu, na rehema….} [6:157]

Na kuwa huongoza kwa yaliyonyooka (madhubuti), Allah amesema: {Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa.} [17:9]

Humuongoza mwanadamu katika njia iliyonyooka katika kila jambo katika maisha yake,

Qur-aan imekusanya kila kitu anachokihitaji mwanadamu; kwani inakusanya misingi ya kanuni, itikadi, hukumu, miamala, maadili, adabu zake na mengineyo, Allah amesema: {…Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote….} [6:38].





## Kitabu Chenye Kukusanya

"Kwa hakika Qur-aan ni kitabu cha elimu, malezi na utamaduni, haina maana kwamba yote yaliyomo ndani yake ni maneno kuhusu faradhi za Swala na Ibada. Mambo mema ambayo Qur-aan inahamasisha Waislamu mambo mema kabisa katika mizani ya maadili mema. Muongozo wa kitabu hiki unaonekana zaidi katika makatazo yake, kama yalivyo wazi katika maamrisho yake pia."

**Sydney Fisher**

Profesa katika Chuo Kikuu cha Ohio-Marekani.

## SUNNAH ZA MTUME (Swala Llahu 'alayhi wasallam)

Allah amemteremshia Mtume wake Qur-aan Tukufu na akampa Wahyi wa Sunnah ya Utume, Allah amesema: {Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa} [53:4]

Nayo ni kama Qur-aan Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: "Jueni mimi nimepewa Kitabu (Qur-aan) na mfano wake pamoja nao, jueni, mimi nimepewa Kitabu (Qur-aan) na mfano wake pamoja nao" (Ahmad). Ni Wahyi kutoka kwa Allah kwa Mtume wake Muhammad (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa sababu Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hazungumzi kwa matamanio, Yeye hufikisha kwa watu aliyoamrishwa, Allah amesema: {…Mimi nafuata niliyo funuliwa tu kwa Wahyi, wala mimi si chochote ila ni mwonyaji mwenye kudhihirisha wazi.} [46:9].

Kwa hiyo Sunnah ni chanzo cha pili katika vyanzo vya Uislamu, nayo ni yote yaliyopokewa kutoka kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) kwa sanadi sahihi inayoungana hadi kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) nayo ni maneno yake, kauli, kukiri au wasifu, nayo ni yenye kusherehesha na



### Sunnah Tukufu

"Hakika Sunnah ing'aayo ya Muhammad imebakia hadi leo hii. Ikifunikwa na ikhlasi sahihi ya kidini, nafsi za mamilioni ya wafuasi wa Sunnah yake wametapakaa kwenye mgongo wa dunia."

**Etienne Denier**

Mchoraji na Mwanafikra wa Kifaransa

kubainisha kwa ajili ya Qur-aan Tukufu; Allah amemuidhinisha yeye abainishe yaliyo ndani ya Qur-aan katika mambo ya jumla, au mahususi, Allah amesema: {…Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri.} [16:44];

Kwa hiyo Sunnah inabainisha Qur-aan na kufafanua ayah zake, na hupambanua hukumu zake za jumla, kama vile Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alivyokuwa akipambanua yaliyokuwa yakiteremka mara nyingine kwa maneno, wakati mwingine kwa vitendo, na wakati mwingine kwa njia zote pamoja.

Huenda Sunnah ikajitegemea bila Qur-aan Tukufu kwa kubainisha baadhi ya hukumu na sheria zake.

Sunnah iliotoharika ndiyo utekelezaji wa vitendo vya Uislamu kwa hukumu, itikadi, ibada, miamala na taratibu zake.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa anatekeleza aliyoamrishwa, na kuyabainisha kwa watu na anawaamrisha kufanya mfano wa matendo yake, Allah amewaamrisha waumini kumfuata yeye (Swala Llahu 'alayhi wasallam) katika matendo yake na katika maneno yake ili imani yao ikamilike, Allah amesema: {Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.} [33:21].



**Qur-aan na Hadithi bega kwa bega.**

"Qur-aan ina kamilishwa na hadithi ambazo ni mtiririko wa maneno yanayofungamana matendo ya Mtume Muhammad (Swala Llahu 'Alayhi Wasallam) na maelekezo yake. Katika hadithi mtu anapata yale yote yaliyokuwa yakitokea kwa Mtume (Swala Llahu 'Alayhi Wasallam). Ni kipengele cha msingi katika tabia zake mbele ya hakika zenye kubadilika katika maisha. Hivyo basi Sunnah ndio yenye kubainisha Qur-aan wala haijitoshi peke yake."

**Jack Rislow**

Mustashrik wa Kifaransa



Masahaba wamenakili na kupokea kutoka kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) matendo ya Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) hadi wale waliokuja baada yao, nao wamepokea hadi kwa waliokuja baada yao kisha wakasajili katika Rejesta (diwani) za Sunnah.

Wapokezi wa Sunnah walikuwa wakishadidia (wakiweka mkazo na msisitizo mkubwa) katika yale waliyokuwa wakipokea kutoka kwao, na wakitaka wale wanaopokea kwao wawe watu walioishi zama moja na wale wanaopokea kutoka kwao, ili isnadi iungane kutoka kwa Rawiy (Mpokezi) wa Hadithi hadi kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kuwa wapokezi wote (walio katika mtiririko wa ile sanadi) ni watu madhubuti (wenye kuaminiwa) na waadilifu, wakweli na waaminifu.

Inapasa kuamini Qur-aan na Sunnah kuwa ndio vyanzo vikuu vya dini ya Uislamu ambavyo yapasa kuvifuata na kuvirejea na kufuata maamrisho yake, kuacha makatazo yake, kuamini habari zake na majina matukufu ya Allah yaliyo ndani yake, sifa zake na matendo yake, na yote aliyoandaa Allah kwa ajili ya mawalii wake waumini, na aliyokamia nayo adui zake makafiri, Allah amesema:



**Muongozo wa Sunnah**

"Kuitekeleza Sunnah ya Muhammad ni kuhifadhi kiini cha Uislamu na kuuendeleza, na kuacha Sunnah ni kuangusha Uislamu. Sunnah ndio msingi wa chuma ambalo juu yake Uislamu umesimama na ukiondoa muundo wake usishangae kuona jengo lile likianguka kama vile nyumba ya vikaragosi."

**Leopold Weiss**

Mwanafikra wa Austria.



{La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.} [4:65]

Na akasema vile vile Allah: {…Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho….} [39:7]

Ni furaha iliyoje kwa atakayefuata njia hii nayo ni njia ya Furaha!!!



### Kukusanywa kwa Sunnah za Mtume.

"Hadithi hizi ambazo mkusanyiko wake unatengeneza Sunnah zimeandikwa kutokana na yaliopokewa kutoka kwa Masahaba au kunakiliwa kutoka kwao kwa umakini mkubwa katika kuzichagua kwake; na kwa namna hii kiasi kikubwa cha Hadithi kilikusanywa."

**Jack Rislow**

Mustashrik wa Kifaransa.



